(2) Kila amri iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha (1) itataia-

(a) jina la gazeti linalohusika na amri hiyo;

(b) majina ya mwenye gazeti, mchapishaji na mtoaji wa gazeti hilo:

Isipokuwa kwamba hakuna amri kama hiyo iliyolewa kwa mujibu wa kifungu cha (1) itakayokuwa batu kwa sababu ya kukosa kutoa maelezo au kutoa maelezo yasiyo sahihi kuhusu mwenye gazeti, mchapishaji au mtoaji wa gazeti au ye yote kati yao.

(3) Iwapo amri imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha (1) kuhusu gazeti lo lote-

(a) mtu ye yote ambaye, tangu tarehe ya kuanza kutumika. atachapisha au kutoa au kuagiza lichapishwe au litolewe gazeti lo lote lililotajwa katika amri hiyo, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa - kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyo, zidi shilingi elfu ishirini au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka minne au kupewa adhabu zote mbili pamoja;

(b) mtu ye yote ambaye, tangu tarehe ya kuanza kutumika, atauza, atachuuza, atagawa, kuweka au kuagiza iwekwe hadhara ya watu nakala yo yote au sebemu ya nakala ya gazeti lililotajwa katika amri hiyo, iwe nakala hiyo au sehemu yake ilichapishwa au kutolewa kabla ya tarehe ya kuanza kutumika au sivyo, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi au kutungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka miwili au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

(4) Kwa madhumuni ya fungu hili "hadhara ya watu" ina maana ya kawaida ya maneno hayo na pia ifahamike kuwa ni pamoja na njia yo yote ambayo watu wana haki ya kupita, jengo, mahali au chombo ambacho watu wana haki ya kukitumia ama bila masharti au kwa malipo, na jengo lo lote au mahali po pote panapotumiwa na watu kwa ajili ya ibada au mikutano au mahakama ambayo watu wote wanakuwa huru kuhudhuria.

SEHEMU YA V

MAKOSA DHIDI YA JAMHURI

26. Kwa madhumuni ya Sehemu hii ya Sheria hii-

"gazeti" ina maana ya kawaida ya neno hilo na pia ifahamike kuwa ni pamoja na mambo yote yaliyoandikwa au kupigwa chapa, na sahani ya santuri yo yote au sahani ya aina nyingine yo yote, hati ya kumbukumbu, ukanda au waya, wa kunasia sauti, Mamu ya picha. za sinema au zana za namna nyingine yo yote zinazoweza kutumika kwa ajili ya kudhihirishia, kutolea au kutangazia fikra au maneno, na kila kitu, iwe chenye asili ya vitu hivyo vili-vyotajwa hapo juu au sivvo, chenye mambo yanayoonekana au ambacho, kutokana na umbile lake au hali yake nyingineyo. au kwa namna nyingine yo yote, chaweza kutumika kwa ajili ya kudhihirisha, kutoa au kutangaza fikra au maneno, na kila nakala au igizo la gazeti lo lote;

"gazeti la majira" maana yake ifahamike kuwa ni pamoja na kila gazeti linalotolewa kwa vipindi maalum au linalotolewa mara kwa mara au kwa mfululizo wa makala yanayotolewa moja moja au mara moja moja;

"gazeti linalochochea uasi" maana yake ni gazeti ambalo ndani yake mna mambo yenye nia ya kuchochea uasi.

27.-(1) Rais akiona kwamba uingizaji nchini wa gazeti lo lote ni kinyume cha manufaa ya umma, aweza, kwa nadhari" yake, kutoa amri ya kupiga marufuku uingizaji nchini wa gazeti hilo, na iwapo gazeti linalohusika ni gazeti la majira, basi aweza, ama kwa amri hiyo au kwa amri nyingine ya baadaye, kupiga marufuku uingizaji nchini wa sehemu yo yote au toleo lo lote lijalo la gazeti hilo.

(2) Rais akiona kwamba uingizaji nchini wa gazeti la mtu ye yote aliyetajwa mahsusi ni kinyume cha manufaa ya umma, aweza, kwa nadhari yake, kutoa amri ama ya kupiga marufuku kabisa au kupiga marufuku yenye masharti yanayoweza kulegezwa ikihitajika, uingizaji nchini wa matoleo yajayo ya gazeti la mtu huyo anayehusika.

28.-(1) Mtu ve yote atakayeingiza nchini, atakayetoa, atakayeza, atakayecheuza, atakayegawa au atakayetengeneza nakala ya gazeti lo lote ambalo uingizaji wake nchini umepigwa Marufuku kwa mujibu wa fungu la 27 au atakayetumia nakala yo yote ya gazeti hilo kwa ajili ya jambo lo lote kati ya mambo hayo yaliyotajwa hapo juu, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa, kwa kosa la kwanza, kututonzwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka miwili au kupe- wa adhabu zote mbili pamoja, na kwa kosa jingine lo lote, kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi na tano au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka mitatu, na hilo gazeti, au nakala. yake, litachu- **kuliwa na Serikali.**

Ufafanuzi
kwa
madhumuni
ya sehemu
hii

Uwezo wa
kupiga
marufuku
uingizaji wa
magazeti
nchini

Makosa
yanayohu-
sika na
magazeti
yaliyopigwa
marufuku
kuingizwa
nchini

(2) Mtu yote ambaye. bila kuwa na sababu inayokubalika kish-
ria. atakuwa na gazeti lo lote, ambalo uingizaji wake nchini umepigwa
marufuku kwa mujibu wa fungu la 27 au atakayekuwa na nakala ya
gazeti hilo, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele,
ya mahakama atapaswa kuadhibiwa, kwa kosa la kwanza, kwa kutozwa
faini isiyoziidi shilingi elfu tano au kufungwa gerezan, kwa muda
usioziidi miezi kumi na mbili au kupewa adhabu zote mbili pamoja, na
kwa kosa jingine lo lote, kutozwa faini isiyoziidi shilingi elfu kumi au
kufungwa gerezani kwa muda usioziidi miaka miwili; na hilo gazeti, au
nakala yake, litachukuliwa na Serikali.

Kupeleka
magazeti
yaliyopig
wa
marufuku
kwa ofisi
utawala au
kwenye
kituo cha
Polisi

29.-(1) Mtu ye yote ambaye atapelekwa pzcti lo lote au nakala
ya gazeti lo lote ambalo uingizaji wake nchini umepigwa marufuku
kwa muiibu wa fungu la 27, bila yeye mwenyewe kujua au kufuatana
na maombi aliyoyatoa kabla ya Uingizaji nchini wa gazeti hilo hauja-
pigwa marufuku, au ambaye atakuwa na gazeti hilo au nakala yake
wakati uingizaji nchini wa gazeti hilo utakapopigwa marufuku, itamla-
zimu, mara tu baada ya kugundua yaliyomo kwenye gazeti hilo, au
ikiwa gazeti hilo, au nakala yake, amelipata kabla ya kutolewa amri
ya kupiga marufuku uingizaji nchini wa gazeti hilo, basi mara tu
baada ya kutolewa amri huyo ya kupiga marufuku, kupeleka. gazeti
hilo au nakala yake kwa Ofisa utawala aliye karibu naye au kwa mkuu
wa kituo cha Polisi kilicho karibu naye na akikosa kufanya hivyo
atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia Mbele ya mahakama
atapaswa kuadhibiwa . kwa kutozwa faini isiyoziidi shilingi elfu tano
au kufungwa gerezani, kwa muda usioziidi miezi kumi na mbili au
kupewa adhabu zote Mbili pamoja, na hilo gazeti, au nakala yake, lita-
chukuliwa na Serikali.

(2) Mtu ye yote ambaye ametimiza masharti ya kifungu cha (1)
ambaye amepatikana na hatia, mbele ya mahakama kwa kosa chini ya
kifungu hicho, hawezi kutiwa hatiani kwa kosa la kuingiza nchini au
kuwa na gazeti hilo, hilo au nakala yake,

Uwezo wa
kukagua
mizigo

30.-(1) Ye yote kati ya maofisa wafuatao, yaani-
(a) ofisa ye yote wa Shirika la posta na simu la Afrika ya Masha-
riki Mwenye cheo kisichopungua daraja la Mkuu wa Posta;
(b) ofisa ye yote wa Idara ya Forodha mwenye ,heo kisichopungua
daraja la Mratibu;
(c) ofisa wa polisi ye yote mwenye cheo kisichopungua daraja la¹
Mkaguzi;
(d) ofisa mwingine ye yote aliyeidhiniwa kwa madhumuni hayo na
Waziri mwenye dhamana ya mambo ya ndani ya nchi,
aweza kuzuia,kufungua na kukagua mzigo au kitu chochote ambacho
anakitilia shaka kwamba ndani yake mna gazeti lo lote au nakala yake
ambayo kwayo ni kosa, kwa mujibu wa fungu la 28 la Sheria hii , kuingi-
za nchini, kutoa. kuuza, kuchuuza, kugawa, kutengenezwa nakala yake
au kuwa nayo, na wakati wa ukaguzi huo, aweza kumweka chini ya
ulinzi mtu ye yote aliye na mzigo huo au kitu hicho ambaye anaingiza
nchini, anagawa au anapeleka kwa posta mzigo huo au kitu hicho,

(2) Iwapo gazeti kama, hilo, au nakala yake, litakuwemo ndani ya mzigo huo au kitu hicho, basi mzigo huo wote au kitu hicho chote chaweza kuchukuliwa na kuhifadhiwa na ofisa huyo na huyo mtu aliyepatikana na mzigo huo au kitu hicho ambaye alikuwa anaingiza nchini au anagawa au anapeleka kwa posta mzigo huo au kitu hicho aweza kukamatwa mara moja na kuchukuliwa hatua za kisheria kwa ajili ya kosa chini ya fungu la 28 au fungu la 29, kadri itakavyokuwa.

31.-(1) "Nia ya kuchochea uasi" ni nia ya-

- (a) kuchochea. chuki au ufidhuli au uasi dhidi ya Jamhuri ya Muungano au Serikali yake; au
- (b) kuchochea wakazi wo wote wa Jamhuri ya Muungano kujaribu kuleta mapinduzi ya kijambazi ya jambo lo lote katika Jamhuri ya Muungano, lililowekwa kwa mujibu wa Sheria;
- (c) kuchochea chuki au ufidhuli au uasi dhidi ya utekelezaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano;
- (d) kuchochea manung'uniko na chuki au uasi miongoni mwa wakazi wa Jamhuri ya Muungano;
- (e) kuchochea chuki na uhasama baina ya vikundi mbali mbali vya wakazi wa Jamhuri ya Muungano.

Nia ya
kuchochea
uasi

(2) Kitendo, maneno au gazeti halitahesabika kuwa ni la kuchochea uasi ikiwa lengo lake ni-

- (a) kuonyesha kwamba Serikali imepotoshwa au imekosea, katika shu-Auli yake yo yote-, au
- (b) kuonyesha makosa au hitilafu katika Serikali au Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kadri mambo hayo yalivyo kwa mujibu wa Sheria, au katika Sheria za nchi au katika utekelezaji wa haki, kwa madhumuni ya kusahihisha au kurekebisha makosa hayo au hitilafu hizo; au
- (c) kuwashawishi wakazi wo wote wa Jamhuri ya Muungano kujaribu, kwa njia zilizo halali kwa mujibu wa Sheria, kuleta mabadiliko ya jambo lo lote lililowekwa kwa mujibu wa Sheria;
- (d) kuonyesha, kwa madhumuni ya kutaka yaondolewe, mambo yo yote yanayochochea au yanayoweza kuchochea chuki na uhasama baina ya vikundi mbali mbali vya wakazi wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Katika kufikiria kama jambo lo lote lilitendwa, maneno yo yote yalitamkwa au hati yo yote ilichapishwa na kutangazwa, kwa nia ya kuchochea uasi, kila mtu atahesabika kuwa. ana jukumu kamili juu ya matokeo yote ya vitendo vyake vyote vya makusudL

32.-(1) Mtu ye yote ambaye-

- (a) atatenda au kujaribu kutenda. au atatarisha kutenda. au atakula njama na mtu ye yote ya kutenda, jambo lo lote kwa nia va kuchochea uasi
- (b) atatamka maneno yo yote kwa nia ya kuchochea uasi;
- (c) atachapisha, kutoa, kuuza, kuchuuza, kugawa au kutengeneza nakala ya gazeti linalochochea uasi:

Makosa ya
kuchochea
uasi

(d) ataingiza nchini gazeti linalochochea uasi, isipokuwa kama bana sababu ya kuamini kwamba gazeti hilo linachochea uasi,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa, kwa kosa la kwanza, kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka miwili au kupewa adhabu zote mbili pamoja, na kwa kosa jingine lo lote, kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi na tano au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka mitatu au kupewa adhabu zote mbili pamoja; na hilo gazeti litachukuliwa na Serikali.

(2) Mtu ye yote ambaye, bila kuwa na sababu inayokubalika kishe-ria, atakuwa na gazeti linalochochea uasi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa, kwa kosa la kwanza, kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi, elfu tano au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au kupewa adhabu zote mbili pamoja, na kwa kosa jingine lo lote, kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka miwili au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

(3) Endapo mtu atashtakiwa kwa mujibu wa kifungu cha (2), basi mahakama itabidi ikubali kuwa kuna utetezi wa kutosha ikiwa wakati alipopata hilo gazeti huyo mshtakiwa hakujua kwamba gazeti hilo lilichochea uasi na kwamba mara tu alipogundua yaliyokuwamo katika gazeti hilo alilipeleka kwa ofisa utawala aliyekuwa karibu naye au kwa mkuu wa kituo cha Polisi kilichokuwa karibu naye.

(4) Mashine ya kupigia chapa yo yote iliyotumika au inayotuhumiwa imetumika kwa ajili ya kupigia chapa au kutengenezea nakala ya gazeti linalochochea uasi yaweza kuchukuliwa au kuzuiliwa na ofisa wa Polisi wakati wa kungojea kusikilizwa shauri na kutolewa hukumu juu ya mtu ye yote aliyeshitakiwa kwa kosa la kuchapisha au kutengeneza nakala ya gazeti linalochochea ulasi; na iwapo mtu ye yote atapatikana na hatia ya kuchapisha au kutengeneza nakala ya gazeti linalochochea uasi, hiyo mahakama yaweza, pamoja na adhabu nyingine yo yote inayoweza kumpa mshtakiwa, kuamuru kwamba hiyo mashine iliyotumika kwa ajili ya kupigia chapa au kutengenezea nakala ya hilo gazeti linalochochea uasi ama ichukuliwe na Serikali kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au ichukuliwe kabisa na Serikali, na mahakama hiyo yaweza kutoa amri kama hiyo hata kama hiyo mashine iliyotumika haikuwa mali ya huyo mshtakiwa.

(5) Mashine ya kupigia chapa iliyochukuliwa na Serikali kwa mujibu wa kifungu cha (4) itauzwa na fedha itakayopatikana, baada ya kuondoa gharama za lazima, itaingia katika Hazma ya Serikali.

(6) Endapo mwenye gazeU, pter4ji au mchapishaji gazed au Mhariri wa gazed atapatikana na hatia kwa kosa la kuchapisha au kutoa gazeti linalochochea uasi, hiyo mahakama yaweza, pamoja na adhabu nyingine yo yote inayoweza kumpa mshtakiwa, na iwe imetoa amri yo yote kwa mujibu wa kifungu cha (4) au sivyoy, kutoa amri ya kupiga marufuku uchapishaji, wa gazeti hilo kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili.

(7) Mahakama yaweza, wakati wote, kutokana na maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baada ya mtu anayehusika kutoa dhamana, kama itahitajika, kwa ajili ya tabia njema, kadri mahakama itakavyoamua, kutangua amri yote iliyotolewa na mahakama hiyo kuhusu kuchukuliwa kwa mashine ya kupigia chapa na Serikali au amri ya kupiga marufuku uchapishaji wa gazeti.

(8) Kabla mahakama haijatoa amri ya kuchukuliwa kwa mashine ya kupigia chapa na Serikali kwa mujibu wa fungu hili itabidi iridhike kwamba mashine hiyo ndiyo iliyotumika kwa ajili ya kupigia chapa au kutengenezea nakala ya hilo gazeti linalochochea uasi.

(9) Iwapo mashine ya kupigia chapa imechukuliwa na Serikali au na Ofisa wa Polisi kwa mmjibu wa fungu hili, basi Mkuu wa jeshi la Polisi, kwa nadhari yake aweza-

- (a) kuagiza kwamba hiyo mashine yote au Sehemu yote ya mashine hiyo iondolewe hapo ilipo na kuwekwa mahali pengine; au
- (b) kuagiza kwamba sehemu fulani ya mashine hiyo izibwe au ifungwe ili kuzuia isitumike:

Isipokuwa kwamba mwenye mashine hiyo au wawakilishi wake watakuwa na haki ya kufika hapo ilipo mashine na kuchukua hatua Yo yote inayohitaiika kwa ajili ya kuzuia mashine hiyo isiharibiwe.

(10) Mkuu wa Jeshi la Polisi au ofisa wa Polisi Mwingine ye yote atakayetokeleza madaraka yake kwa mujibu wa fungu hili hatakuwa na lawama kwa ajili ya hasara yote itakayotokea inayohusika na mashine hiyo, iwe hasara hiyo imesababishwa na uzembe au kwa namna nyingine yote, isipokuwa kama hasara hiyo imetokana na uharibu wa makusudi wa hiyo mashine.

(11) Mtu ye yote, atakayetumia au kujaribu kutumia mashine ya kupigia chapa iliyochukuliwa na Serikali au na ofisa wa polisi kwa mujibu wa kifungu cha (4) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyovidi shilingi elfu kumi na tano au kufungwa gereza kwa muda usiozidi miaka mitatu au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

(12) Mtu ye yote atakayechapishwa au kutoa gazeti kinyume cha amri iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha (6) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi na tano au kufungwa gereza kwa muda usiozidi miaka mitatu au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

(13) Katika fungu hii "mashine ya kupigia chapa" maana yake ni pamoja na mitambo ya kupigia chapa, mitambo ya kutengenezea nakala au picha au mashine au zana ya namna nyingine yote zinazotumika kwa ajili ya kupigia chapa au kutengenezea nakala za magazeti na vifaa vinavyoandamana na mashine au mitambo kama hivo.

Mashauri ya jinai	<p>33.-(1) Mashtaka kwa ajili ya kosa lo lote chini ya, fungu la 32 ni lazima yafunguliwe ndani ya miezi sita tangu kosa lilipotendeka:</p> <p>isipokuwa kwamba ikiwa mtu yeyote-</p> <p>(a) ametenda kosa hilo akiwa nje ya, Jamhuri ya Muungano; au</p> <p>(b) ameondoka Tanganyika ndani ya miezi sita baada ya kutenda kosa hilo,</p> <p>mashtaka, kwa ajili ya kosa hilo itabidi yafunguliwe ndani ya miezi sita tangu siku ambayo mtu huyo ataingia kwa Mara ya kwanza au atarejea katika Jamhuri ya Muungano baada ya-</p> <p>(i) kutenda kosa hilo; au</p> <p>(ii) kuondoka Tanganyika.</p> <p>kadri itakavyokuwa.</p> <p>(2) Mtu hawezi kushtakiwa kwa ajili ya kosa lo lote chini ya fungu la 32 ila iwe kimepatikana kibali cha maandishi cha Mkurugenzi wa Mashtaka.</p>
ushahidi	<p>34. Hapana mtu ye yote atakayetangazwa hatiani kwa kosa lo lote chini ya fungu la 32 kutokana, na ushahidi wa mtu mmoja tu ambao haukuungwa mkono na ushahidi wa mtu au watu wengine.</p>
Ufafanuzi wa tendo la dhahiri	<p>35. Ikiwa, kuhusu kosa lo lote miongoni mwa makosa ya yotajwa na kufafanuliwa katika Sehemu hii ya Sheria hii, ni lazima kwamba nia ya kutenda kosa, hilo ibadilishe kwa tendo la dhahiri, basi kila tendo la kula njama, na mtu ye yote kwa makusudi ya, kutimiza nia hiyo, na tendo jingine Jo lote la Intu ye yote aliyekula njama hiyo lenye shabaha ya kutimiza na hiyo, litahesabika kuwa ni tendo la dhahiri linalobainisha nia hiyo.</p>
Utangazaji wa habari za uwongo zinazoweza zinazoweza kuwashutusha watu na kuwatia woga na wasi wasi	<p>36.(1) Mtu ye yote atakayetangaza au kueneza habari yo yote ya uwongo, Uzushi au taarifa ambayo yaweza kuwatia watu woga na wasi wasi au kuchafua amani katika nchi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu kumi na tano au kufungwa gere-zani kwa muda usiozidi miaka mitatu au kupewa adhabu zote mbili pamoja</p> <p>(2) Iwapo mtu ye yote atashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu cha (1) mahakama itabidi ikubali kuwa kuna utetezi wa kutosha ikiwa mshtakiwa atathibitisha kwamba kabla ya kutangaza au kueneza habari au taarifa ya aina iliyoelezwa katika kifungu cha (1) alichukua hatua madhubuti za kuhakikisha ukweli wa mambo na kwamba matokeo yake yalimfanya asadiki kwamba habari au taarifa hiyo ilikuwa ya kweli.</p>

37.-(1) Mtu ye yote ambaye, bila sababu ya maana. inayokubalika. Kuchochea kisheria, atachapisha, kutangaza, kueneza. au kutamka, maneno yo yote kwenye mkutano kwa makusudi ya, kushawishi watu kwamba inafaa au kuna. haja ya, kutenda, jambo lo lote kinyume cha, Sheria kwa ajili ya-

(a) kuleta, mauti au madhara. ya, mwili kwa, mtu ye yote au aina yo yote ya watu au jamii ya, watu; au

(b) kuharibu au kuteketeza, mali yo yote, atakuwa, ametenda kosa na akipatikana na hatia. mbele ya mahakama atapaswa. kuadhibiwa kwa. kutozwa. faini isiyozidi shilingi elfu kumi na tano au kufungwa gerezani kwa. muda, usiozidi miaka, mitatu au kupewa, adhabu zote mbili pamoja.

(2) Kwa madhumuni ya fungu hili "mkutano" maana yake ni mku-sanyiko wa watu watatu au zaidi.

(3) Mtu hawezi kushtakiwa, kwa ajili ya kosa. chini ya. fungu hili i la, iwe kimepatikana kibali cha maandishi cha. Mkurugenzi wa. Mashtaka.

SEHEMU YA VI

KASHFA

38. Mtu ye yote ambaye, bila kuwa, na. haki yo yote kwa. mujibu wa Sheria, atatangaza, mambo yenye kashfa kuhusu mtu mwingine, kwa kuchapisha, kuandika, kuchora, kutumia, kinyago au kwa njia, nyingine yo yote isipokuwa. kwa. ishara peke yake, manono ya. mdomo au sauti nyingineyo, kwa makusudi ya, kumkashifu mtu huyo, atakuwa, amenda, kosa liitwalo "kashfa"

Ufafanuzi
wa kashfa

39. Mambo yenye kashfa, ni mambo ambayo yaweza. kuharibu sifa ya mtu ye yote kwa kumfanya. achukiwe, adharauliwe au afanyiwe kejeli au yanayoweza kumharibia mtu kazi yake kwa, kuchafua jina. lake au kumvunjia, heshima yake, na ni mambo kama wakati yanapotangazwa hayo nianibo yenyo kashfa huyo intu aiiayekasWfiwa yu hai au amefariki dunia:

Ufafanuzi
wa mambo
yenye kashfa

Isipokuwa kwamba mtu hawezi kushtakiwa. kwa, kosa. la, kutangaza mambo yenye kashfa. yanayomhusu mtu aliyefariki i la iwe kimepatikana kibali cha, maandishi cha Mkurugenzi wa Mashtaka.

40.-(1) Mtu husemekana. ametangaza. kashfa ikiwa amef,anya au amecha kufanya jambo, lo lote linalowezesha hiyo kashfa ifahamike au iwcze kufahamika kwa huyo mtu allyekashifiwa au mtu mwingine ye yote kwa njia ya kuona, kusoma, kusikia maelezo, kuvokea au kwa namna nyingine yo yote kupata habari za hiyo kashfa iliyomo, kwenye gazeti au hati nyingineyo ifivopigiva chapa, maaidish,, picha au mchoro, kinyago au kitu kingine cho chote chenye hayo mambo yenye kashfa.

ufafanuzi
wa utanga-
zaji

(2) Kwa makusudi ya kufikiria kama, kashfa imetangazwa au la, si lazima, kwamba maelezo yake yawe yametolewa kwa wazi wazi kabisa au kikamilifu; na inato,sha kama hiyo kashfa inaeleweka kuwa inamhusu huyo mtu aliyekashifiwa kutokana na maelezo ya kashfa yenyewe au kutokana na mambo mengine yasiyofungamana na hayo, maelezo ya kashfa au kutokana na baadhi ya maelezo hayo na baadhi ya mambo hayo mengine.

Ufafanuzi wa utangazaji usio halali

41. Kwa madhumuni ya sehemu hii ya Sheria hii, utangazaji wa mambo yenye kashfa utahesabika kuwa si halali isipokuwa kama-

- (a) mambo yenyewe ni ya kweli na yalitangazwa kwa manufaa ya umma; au
- (b) utangazaji wa mambo hayo umehalalishwa na mojawapo ya masharti yaliyoelezwa katika mafungu yanayofuata ya Sehemu hii ya Sheria hii.

Utangazaji wa mambo yeriye kashfa ni halali ikiwa masharti fulani yametimi-

42.-(1) Utangazaji wa mambo yenye kashfa utahesabika kuwa ni halali kabisa, na hapana mtu ye yote anayeweza kuadhibiwa chini ya Sheria hii kwa ajili ya utangazaji wa mambo hayo, kwa Mujibu wa masharti yafuatayo, yaani-

- (a) ikiwa mambo hayo yanatangazwa na Rais. Serikali au Bunge katika hati au shughuli yote ya Serikali; au
- (b) ikiwa mambo hayo yanatangazwa katika Bunge na Rais, Serikali, mjumbe ye yote wa Bunge au Spika; au
- (c) ikiwa mambo hayo yanatangazwa kwa amri ya Rais au Serikali; au
- (d) ikiwa mambo hayo yanatangazwa kuhusu Mtu ye yote ambaye anatakiwa kufuata Sheria na kanuni za kikosi cha Wanamaji au kikosi kingine cho chote cha jeshi la ulinzi la nchi, na mambo hayo yametangazwa kuhusu tabia ya mtu kama huyo. na yanatangazwa na mtu ye yote aliye na mamlaka juu ya huyo mwana-jeshi kuhusu tabia hiyo; au
- (e) ikiwa, mambo hayo yanatangazwa wakati wa kusikilizwa. kwa shauri lo lote mahakamani na yanatangazwa na mtu anayeshiriki katika, shauri hilo kama. jaji an hakimu au kamishna au wakili au mzee wa, baraza, au shahidi au mshtaki au mshtakiwa au. mdai au mdaiwa; au
- (f) ikiwa mambo hayo yanayotangazwa ni taarifa. ya kweli na, sahihi ya jambo lo lote lililosemwa, lilitendwa au lililotangazwa katika, Bunge; au
- (g) ikiwa, huyo mtu anayetangaza mambo hayo ana, jukumu. kwa mujibu wa Sheria. la. kutangaza, mambo hayo.

(2) Ikiwa utangazaji wa, mambo yenye kashfa. unahesabika kuwa ni halali kabisa, bas, kwa madhumuni ya Sehemu hii ya Sheria. hii, itakuwa ni mambo kama, mambo hayo ni ya kweli au ya uwongo, na kama inajulikana au haijulikani au haisadikiwi kuwa mambo hayo ni ya kweli au ya uwongo, na kama, yametangazwa kwa nia safi au Sivyo:

Isipokuwa kwamba hakuna jambo lo lote katika, fungu hili litakalomsalimisha mtu ye yote na jukumu la kuadhibiwa kwa mujibu wa Sehemu nyingine yo yote ya Sheria hii an kwa mujibu wa Sheria nyingine yo, yote inayotumika katika Tanganyika.

43. Utangazaji wa mambo yenye kashfa utahesabika kuwa ni haw kwa masharti raaalum ikiwa mambo hayo yanatangazwa kwa nia safi na ildwa uhusiano baina ya, mtu anayetangaza na mtu anayetangaziwa mambo hayo, unamfanya, huyo mtangazaji kuwa na jukumu la kumtangazia huyo, mtu mwingine ama kwa mujibu wa Sheria an kufuatana na mila au kanuni za mwenendo bora katika jarnii kwa jumla an ikiwa huyo, mtangazaji anatekeleza masilahi yake yaliyo halali kwa kutangaza mambo hayo, ila kwa shard kwamba katika hali kama hiyo huo utangazaji hauzidi mpaka kwa namna yo yote, na. pia utangazaji utahesabika, kuwa ni halali kwa masharti maalum kwa mujibu wa masharti yafuatayo, yaani-

Utangazaji wa mambo yenye kashfa si halali ila kwa masharti maalum

- (a) ikiwa mambo yanayotangazwa ni taarifa ya kweli na sahihi ya jambo lo lote lililosemwa, lililotendwa au lililoonekana katika shauri lo lote la madai au la jinai linalosikilizwa mahakamani:

Isipokuwa kwamba iwapo mahakama. itapiga marufuku utangazaji wa jambo lo lote lililosemwa au lililoonekana katika mahakama, hiyo kwa sababu kwamba jambo hilo linachochea uasi, ni ovu, au ni la kukufuru basi utangazaji wa jambo kama hilo hautahesabika kuwa ni halali; au

- (b) ikiwa mambo yanayotangazwa yametokana na nakala au muhtasari halisi wa mambo yaliyopata kutangazwa wakati uliopita, .:na ikiwa utangazaji wa mambo hayo wakati uliopita mlikuwa halali kwa mujibu wa fungu la 42 la Sheria hii; au
- (c) ikiwa mambo hayo, ni maoni yaliyotolewa kwa, nia safi kuhusu vitendo vya kikazi vya mtu ye yote mwenye madaraka katika shughuli za mahakama, Serikali au za chombo kingine cho chote cha umma au kuhusu tabia yake binafsi kwa kadri tabia, hiyo inavyoonekana katika vitendo vyake vya, kikazi; au
- (d) ikiwa mambo hayo ni maoni yaliyotolewa kwa nia safi kuhusu vitendo vya mtu ye yote vinavyohusika na swala au jambo lo lote linalohusu umma, au kuhusu tabia yake binafsi kwa kadri tabia hiyo, inavyoonekana katika vitendo kama hivyo; au
- (e) ikiwa mambo hayo ni maoni yaliyotolewa kwa nia safi juu ya tabia ya mtu ye yote kama ilivyoonekana kwenye ushahidi uliotolewa katika shauri lo lote la kisheria lililosikilizwa hadharani, kama ni shauri la madai au la jinai, kuhusu tabia ya mtu ye yote ambaye katika shauri hilo anashiriki kama mshtaki au mshtakiwa, mdai au mdaiwa, shahidi au anashiriki kwa namna nyingine yo yote, au kuhusu labia binafsi kwa, kadri tabia hiyo inavyoonekana kwa jinsi ilivyoonekana katika fasili hii- au

- (f) ikiwa mambo hayo ni maoni yaliyotolewa kwa nia safi kuhusu ubora wa kitabu cho chote, maandishi, picha au mchoro, hotuba au shughuli nyingineyo yo yote, maonyesho au tendo lililotangazwa au kutendwa kwa hadhara au lililotendwa au kutolewa hadharani kwa ajili ya kutaka kupata maoni ya watu, au kuhusu tabia binafsi ya mtu ye yote anayehusika na lo lote katu ya mambo hayo yaliyotaiwa kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika mambo hayo; au
- (g) ikiwa mambo hayo ni lawama iliyotolewa na mtu kwa nia, safi kuhusu vitendo vya mtu mwingine katika jambo lo lote anibalo huyo aliyetoa lawama ana mamlaka nalo, ama kwa mujibu wa mkataba au vinginevyo, na kwa kadri anavyohusika huyo aliyelaumiwa, au kuhusu tabia binafsi ya mtu huyo aliyelaumiwa kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika vitendo hivyo; au
- (h) ikiwa mambo hayo ni malalamiko au mashtaka yaliyotolewa na mtu kwa nia safi dhidi ya mtu mwingine kuhusu vitendo vya mtu huyo mwingine katika jambo, lo lote, au kuhusu tabia yake binafsi kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika vitendo hivyo na ikiwa malalamiko au mashtaka hayo yametolewa mbele ya mtu ambaye ana mamlaka, ama kwa mujibu wa mkataba au vinginevyo, juu ya mtu huyo aliyelaumiwa au kushtakiwa kuhusu vitendo vyake au tabia yake, au malalamiko au mashtaka hayo yametolewa mbele ya mtu ambaye kwa mujibu wa Sheria ana mamlaka yo kuchunguza au kupokea malalamiko yanayohusiika na vitendo au tabia kama hiyo; au
- (i) ikiwa mambo hayo yanatangazwa kwa nia safi kwa ajili ya kulinda haki au masilabi ya mtu huyo, anayetangaza, mambo, hayo, au, haki au masilahi ya mtu anayetangaziwa mambo hayo au haki au masilahi ya mtu mwingine ye yote ambaye anahusiana na huyo mtu anayetangaza mambo hayo.

44. Utangazaji wa mambo yenye kashfa hautahesabika kuwa ume-fanywa na mtu ye yote kwa nia ". kwa madhumum ya fungu la 43. kama itaonekana ama-

Ufafanuzi
wa nia safi

- (a) kwamba mambo hayo hayakuwa ya kweli, na kwamba huyo mtangazaji hakusadiki kwamba yalikuwa ya kweli; au
- (b) kwamba mambo hayo hayakuwa ya kweli na kwamba huyo Mtangazaji aliyatangaza bila kuchukua hatua yo yote madhubuti ya kuhakikisha kama mambo hayo yalikuwa ya kweli au ya uwongo; au
- (c) kwamba, alipoyatangaza mambo hayo huyo mtangazaji alikusudia kumvunjia heshima huyo mtu aliyekashifiwa kwa kiasi au kwa namna ambayo haikuwa lazima wala kuhitajika kwa manufaa ya umma au kwa ajili ya kulinda haki zake au maslahi yake ambayo anadai kuwa ndio msingi wa kutaka utangazaji wake uhesabike kama ni utangazaji ulio halali kwa Mujibu wa Sheria

45. Iwapo itathibitishwa na upande wa mshtaka kwamba. hayo mambo yeyiye kashfa. yalitangazwa kwa namna. na. katika. hah ambayo utangazi huo ulistahm kuhesabika, kuwa. umefanywa. kwa nia. safi, basi utangazaji huo utahesabika kuwa ubfanywa kwa ma. safi mpaka. itaka. podhihirika kuwa huo sio ndio ukweli wa mambo, ama kutokana na. maelezo ya kashfa yenyewe au kutokana na. ushahidi wa. upande wa mashtaka.

Mambo yanayobainisha nia safi

46. Mtu ye yote ambaye, bila kuwa na. sababu iliyo halali kwa mujibu wa Sbefla. atatangan au kueneza jambo lo lote linalokusudiwa lisomwe, au kitu kingine cho chote kinachoweza kuonekana, kinachoweza. kuvunja heshima kukebehi au kuchochea. chuki au dharau dhidi ya mtawala au kiongozi ye yote wa nchi nyingine, balozi au mtu mashahuri mwingine ye yote wa nchi nyingine kwa. makusudi ya. kuvuruga amani na. uhusiano mwema. baina ya. Jamhuri ya Muungano na. hiyo nchi nyingine, atakuwa ametenda kosa. la. kashfa.

Marufuku kukashifu watu mashuhuri wa nchi nyingine

47. Mtu ye yote atakayepatikana na. hatia kwa. kosa la kashfa chini ya Sheria hii atapaswa. kuadhibiwa. kwa. kutozwa faini isiyoziidi shilingi elfu kumi, au kufungwa, gerezani kwa muda. usioziidi miaka. miwili au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

Adhabu kwa kosa la kashfa

SEHEMU YA VII

MASHARTI MENGINEYO, KUFUTA SHERIA YA ZAMANI NA MABADILIKO YA SHERIA ZA ZAMANI

48. Iwapo, kosa lo lote chini ya Sheria. hii au Kanuni zilizowekwa kwa. mujibu wa Sheria. hii litatendwa, na. kampuni au shirika jingine lo lote, au na chama, umoja au kikundi cha watu, basi pamoja na kampuni hiyo au shirika hilo jingine, au chama. umoja au kikundi cha watu, kila. mtu ambaye wakati kosa hilo lilipotendeka. alishiriki au kuhusika. kama. mkurugenn au ofisa katika uongozi au uendeshaji shughuli za hiyo kampuni au shirika jingine, au chama, umoja au kikundi cha watu, atakuwa vile vile ametenda kosa hilo na atapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria na kuadhibiwa vilivyo, isipo, kuwa kama atathibitisha na kuiridhisha mahakama kwamba hakujua wala asingaliweza kutumia hekima yo yote ya kumwezesha kujua utendaji wa kosa hilo.

Makosa yanayotendwa na mashirika, vyama, n.k,

49. Iwapo kosa lo lote chini ya Sheria hii au Kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria hii litatendwa na mtu ye yote ambaye ni mwakilishi au mtumishi wa mtu mwingine, basi pamoja na huyo mwakilishi au mtumishi, huyo mtu aliyewakilisha madaraka yake au huyo mwajiri atakuwa vile vile ametenda kosa hilo na atapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria na kuadhibiwa vilivyo, isipokuwa kama atathibitisha na kuidhinisha mahakama kwamba hakujua wala asingaliweza kutumia hekima yo yote ya kumwezesha kujua utendaji wa kosa hilo.

Dhima ya mwajiri au mtu anayewakilisha madaraka yake

Utaratibu wa kupeleka taarifa au hati za kuitwa shaurini

50. Hati ya kuitwa shaurini au taarifa yo yote iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria hii au Kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria hii itahesabika kuwa imetolewa na kumfikia mtu anayehusika ikiwa itapelekwa kwake, kwa mkono au kwa barua ya rejesta; na iwapo aliyepolekwa hati au taarifa hiyo ni kampuni au shirika jingine, au chama, umoja au kikundi cha watu, basi hati au taarifa hiyo itahesabika kuwa imetolewa na kumfikia anayehusika ikiwa itapelekwa kwa mkono kwa katibu, mkurugenzi au ofisa mwingine ye yote au kwa mtu mwingine ye yote anayeqfiiriki au kuhusika katika uongozi au uendeshaji wa kazi na shughuli za. hiyo, kampuni au shirika jingine, au chama, umoja au kikundi cha watu, au ikiwa hati au taarifa hiyo itapelekwa kwa barua ya rejesta kwa kutumia anwani ya ofisi iliyoandikishwa au ya mahali pa kazi pa hiyo kampuni, shirika, chama, umoja au kikundi cha watu.

Mamlaka ya mahakama Sura ya 20

51. Bila kujali masharti ya fungu la 7 la Sheria ya Utaratibu wa Mashauri ya Jinai, mahakama ya wilaya inaposikiliza mashauri chini ya uongozi wa hakimumu wa wilaya au chini ya uongozi wa hakimumu mkazi itakuwa na manaka ya kusikiliza shauri lo lote la mtu aliyeshitakiwa kwa kosa lo lote chini ya Sheria hii na itakuwa na uwezo wa kutoa kima cha juu kabisa cha adhabu iliyowekwa, kwa ajili ya kosa linalohusika.

Ukomo wa dhima ya watumishi wa Serikali

52. Hapana mtu ye yote anayeweza kufungua mahakamani shauri lo lote la madai dhidi ya mtumishi wa Serikali ye yote kwa ajili ya jambo lo lote ambalo mtumishi huyo ametenda au ameacha kutenda katika kutekeleza madaraka yake chini ya Sheria hii.

Kanuni

53. Waziri aweza kuweka Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni na masharti ya Sheria hii, na bila kuathiri uwezo huo wa jumla ulioelezwa hapo juu Waziri aweza kuweka. Kanuni-

- (a) zitakazoeleza aina za fomu. madaftari, kumbukumbu, inaombi, taarifa na dhamana, na fomu za aina nyingine zo zote zitakazotumika kwa mujibu wa Sheria hii;
- (b) zitakazotaja aina ya maelezo na marnbo mengine yo yote yatakayoandikwa kwenye madaftari;
- (c) zitakazotaja mahali zitakapohifadhiwa nakala za magazeti na kueleza namna ya kuhifadhi nakala za magazeti zilizopelekwa kwa Msajili kwa mujibu wa Sheria hii, au kueleza namna nakala hizo za magazeti zitakavyotumika kwa mujibu wa Sheria hii;
- (d) zitakazotaja aina ya habari, zitakazotolewa au kupelckwa kwm, Msajili kama kumbukumbu au vinginevyo
- (e) zitakazotaja aina za taarifa na mambo mengine. yatakayotangazwa na Msajili na kueleza namna ya kutoa matangazo kama hayo-

- (f) zitakazotaja viwango vya ada zitakazotozwa kwa mujibu wa Sheria hii;
- (g) zitakazoeleza mambo mengine yo yote ambayo yanatakiwa au yanaruhusiwa kuelezwa katika Kanuni kwa mujibu wa Sheria hii.

54. Sheria ya Magazeti ya zamani sasa imefutwa.

Kufuata
Sheria
ya zamani
Sura ya 229

55. Sheria ya Kanuni za Jinai inabadilishwa ifuatavyo-

Mabadiliko
kwenye
Sheria
ya Kanuni
za jinai
Sura ya 16

- (a) katika Sura ya VII (ambayo inahusika na makosa ya uhaini na makosa mengine dhidi ya Jamhuri)-
- (i) kwa kufuta katika mstari wa pili wa fungu la 50 maneno "Kwa madhumuni ya mafungu ya 51, 52, 53, 54, 55, 56, 57 na 58 ya Sheria hii-" na kuandika badala yake maneno "Kwa madhumuni ya Sura hii-"; na kufuta ufafanuzi wa maneno "kuingiza nchini" na "maeneo ya maji yaliyomo ndani ya mipaka"; na
- (ii) kwa kufuta mafungu ya 51, 52, 53, 54, 56, 57, 58, 63 na 63A;
- (b) katika Sura ya VIII (ambayo inahusika na makosa yanayohasid uhusiano na nchi nyingine), kwa kufuta fungu la 64', na
- (p) katika Sura ya XVIII (ambayo inahusika na kashfa), kwa kufuta mafungu ya 187, 188, 189, 190, 191, 192, 193 na 194.

SEHEMU YA VIII

UTARATIBU MAALUM KUHSU USIKILIZAJI WA MASHAURI YA KASHFA

KATIKA MASHAURI YA MADAI

56.-(1) Kwa madhumuni ya Sehemu hii "mahakama" maana yake ni Mahakama. Kuu, mahakama, ya hakimu mkazi au mahakama ya wilaya inayoongozwa na hakimu wa wilaya mwenye uwezo wa kusikiliza mashauri ya madai na kila inapotajwa mahakama ya wilaya ifahamike kuwa ni mahakama ya wilaya inayoongozwa na hakimu wa wilaya mwenye uwezo wa kusikiliza mashauri ya madai.

Ufafanuzi
kwa madhu-
muni ya
Sehemu
hii na
ukomo wa
matumizi
ya sehemu
hii

(2) Masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Sheria hii yatatumika kwa ajili ya masharti yote ya madai yanayohusu kashfa kutokana na jambo lolote lililochapishwa kwenye gazeti na hayatumika kwa ajili ya mashauri ya aina nyingine yo yote.

Utaratibu
wa Maha-
kama
na wazee
wa
baraza
kusikiliza
mashauri

57.-(1) Bila kujali masharti yaliyomo katika Sheria nyingine yo yote inayotumika ambayo yanaeleza utaratibu wa kusikiliza mashauri katika mahakama, mashauri yote yanayohusika na matumizi ya masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Sheria hii yatasikilizwa na mahakama ikisaidiwa na wazee wa baraza wasiopungua watatu wenye uwezo na sifa bora, na kwa kufuata utaratibu ulioelezwa katika fungu hili.

(2) Katika mashauri yote yanayohusika na matumizi ya masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Sheria hii, baada ya ushahidi wa pande zote mbili kutolewa, mahakama itatoa maelezo, kwa muhtasari, ya ushahidi wote uliotolewa na itamwomba kila mzee wa baraza atoe maoni yake juu ya shauri lote kwa jumla na juu ya jambo maalum lo lote linalohusika na ushahidi ambalo litatajwa na mahakama, na mahakama itaandika kumbukumbu ya maoni hayo.

(3) Wakati wa kutoa hukumu yake katika mashauri yo yote yanayohusika na matumizi ya masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Sheria hii mahakama haitalazimika kufuata maoni ya wazee wa baraza.

(4) Hakuna jambo lo lote katika fungu hili ambalo litafahamika kuwa litawazuia wazee wa baraza, au ye yote kati yao, kwenda faragha kwa ajili ya kufikiria maoni yao ikiwa watapenda kufanya hivyo au kwamba litawazuia wazee wa baraza, au yeyote kati yao, kushauriana juu ya maoni yao ama wakati wakiwa faraghani au wakati shauri linaposikilizwa.

(5) Jaji Mkuu aweza, baada ya kupata kibali cha Waziri mwenye dharnana ya mambo ya Sheria, kuweka Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya fungu hili na bila kuathiri uwezo huo wa jumla ulioelezwa hapo juu, jaji Mkuu aweza kuweka Kanuni-

- (a) zitakazotaja sifa za wazee wa baraza;
- (b) zitakazotaia viwango vya posho watakatayolipwa wazee wa baraza;
- (c) zitakazoweka masharti kwa makusudi ya kuhakikisha kwamba wazee wa baraza watahudhuria mahakamani na ambayo yata. tumika kwa ajili ya uendeshaji wa shauri linalosikilizwa endapo wazee wa baraza wote, au ye yote kati yao, hawataweza kuhu. dhuria mahakamani;
- (d) zitakazoeleza au kutaia jambo jingine lo lote ambalo Jaji Mkuu ataona lahitajika au lafaa kuelezwa au kutajwa kwa makusudi ya utekelezaji bora wa masharti ya Sehemu hii ya Sheria hii.

(6) Kanuni zote zitakazowekwa kwa mujibu wa kifungu cha (5) zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na zitahesabika kuwa zina nguvu ya kisheria sawa na masharti yaliyomo katika Sheria hii

58. Isipokuwa kama imeelema vinginevyo katika Schemu hii ya Sheria hii au katika Kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa fungu la 57, hakuna jambo lo lote filioellema katika Seheinu hii ya Sheria hii ambalo litahesabika kuwa-

- (a) linaathiri matumizi ya masharti ya Sheria nyingineyo yo yote yanayohusika na mamlaka ya mahakatna; au
- (b) linabadilisha au kurekebisha kwa namna nyingine yo yote utaratibu maalum au jambo jingine lo lote kuhusu usikilizaji wa mashauri yanayohusika na matumizi ya masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Sheria hii ikiwa maelezo ya huo utaratibu Maalum au hilo jambo jingine yamo katika Sheria ya Utaratibu wa Mashauri ya Madai au katika Sheria nyingine yo yote.

Imepitishwa katika Bunge la Taifa tarehe kumi na sita Machi, 1976.

Kuhifadhi wa kwa utaratibu wa kusikiliza mashauri ya madai uliowekwa na Sheria ya Utaratibu wa mashauri ya madai na sheria nyinginezo

Sheria za 1966, Na. 49

